



SCCULT

SCCULT (1992) LIMITED

The Savings and Credit Cooperative Union League of Tanzania (1992) Limited P.O.

Box 20640- email: info@sccult.tz, Website: www.sccult.tz TEL. +255 222 185 548/9

Ushirika Tower Lumumba Street, 16 Floor – DAR ES SALAAM – TANZANIA

SCCULT/AGM/2024/VOL.I/001

AGOSTI 28, 2024


KWA SACCOS ZOTE WANACHAMA WA
SCCULT (1992) Ltd
TANZANIA-BARA.

**YAH: TANGAZO LA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA BODI YA SCCULT
(1992) LTD KWENYE MKUTANO MKUU MWAKA WA ISHIRINI NA
SABA (27)**

1. Napenda kuwataarifu kuwa kutakuwa na Uchaguzi wa Viongozi wa Bodi ya SCCULT (1992) Ltd katika *Mkutano Mkuu wa mwaka wa Ishirini na saba* wa wanachama wa SCCULT (1992) Ltd utakaofanyika tarehe 25 Oktoba, 2024 jijini Mwanza katika ukumbi wa Mamlaka ya Maji safi na usafi wa Mazingira (MWAUWASA) jijini Mwanza.
2. Kwa wale ambao watavutiwa kuomba nafasi za Uongozi wanatakiwa kuhakikisha majina yao yametambuliwa na SACCOS zao kama wajumbe wa Mkutano Mkuu wa SCCULT (1992) Ltd na kujaza vizuri fomu na kuwasilisha pamoja na viambatanisho vingine (*Wasifu na nakala zilizo dhibitishwa za vyeti vya elimu na vingine vitakavyohitajika*). Fomu pamoja na viambatanisho viwasilishwe kwenye Ofisi za SCCULT (1992) Ltd Makao Makuu (Jengo la Ushirika, Ghorofa namba 16) au kwenye Ofisi za Warajis Wasaidizi au Maafisa Ushirika.
3. Vyama wanachama wa SCCULT (1992) Ltd mnapaswa kuzingatia taratibu zote za Uchaguzi kama zilivyoelekezwa na Sheria, Kanuni na Masharti.

Aidha kutekeleza taratibu za ulipaji wa ada ya mwaka, uwekezaji na michango mingine yote iliyoamuliwa na Mikutano Mikuu ya wanachama.

4. Ratiba ya uendeshaji wa Uchaguzi huo imeambatanishwa na Tangazo hili.



Mwl. Aziza A. Mshana

MWENYEKITI WA BODI

NAKALA:

1. MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA,
TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA,
S.L.P 201, DODOMA,
TANZANIA. (Kwa taarifa na uratibu)
2. MRAJIS MSAIDIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA (M),
OFISI YA MKUU WA MKOA,
S.L.P 5429, DAR ES SALAAM,
TANZANIA. (Kwa taarifa na uratibu)
3. WARAJIS WASAIDIZI,
MIKOA YOTE TANZANIA BARA (Kwa taarifa na usaidizi wa taratibu za Uchaguzi)
4. MAAFISA USHIRIKA HALMASHAURI,
ZOTE TANZANIA BARA. (Kwa taarifa na usaidizi wa taratibu za Uchaguzi)

RATIBA YA UCHAGUZI WA VIONGOZI

TAREHE	TUKIO
28 Agosti-25 Septemba, 2024	Kuchukua na urejeshaji wa fomu za uchaguzi wa kwenye Ofisi za SCCULT (1992) Ltd, Warajis Wasaidizi na Maafisa Ushirika.
Septemba 26- 30, 2024	Kuandaa taarifa za wagombea kwenye maeneo yote na kuwasilisha TCDC Makao Makuu kwaajili ya taratibu nyingine za Uchaguzi.
Oktoba 01-24, 2024	Taratibu wa upekuzi wa wagombea, usaili (kuhojiwa) na maandalizi ya jumla ya Uchaguzi.
Oktoba 25, 2024	Mkutano Mkuu wa Ishirini na saba (27) na Uchaguzi wa Viongozi